JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI

NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 1014

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I - II

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-820-0

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I - II nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

Kamishna wa Elimu

MUHTASARI WA SOMO LA MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI NA DARASA LA I – II

2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-820-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255-735041168/ +255-735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I – II.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa sehemu ya muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

Yaliyomo

Orodha ya Majedwali iv
Vifupisho v
Shukurani vi
1.0 Utangulizi 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu 2
    3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu 2
    3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji 4
    6.1 Mkufunzi 4
    6.2 Mwalimu tarajali 4
    6.3 Mzazi 5
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji 5
9.0 Upimaji 6
10.0 Idadi ya Vipindi 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji 7
Mwaka wa Kwanza 8
Mwaka wa Pili 15
Bibliografia 20

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Mwaka wa Kwanza na wa Pili....3
Jedwali Na. 2: Alama za Upimaji Endelevu....6
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza....8
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili....15

Vifupisho

TEHAMA Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

TET Taasisi ya Elimu Tanzania

Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I – II yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za umma na zisizo za umma. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

1.0 Utangulizi

Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Elimu ya Awali na Darasa la I – II ni la lazima kwa mwalimu anayetarajiwa kwenda kufundisha Elimu ya Awali na Darasa la I – II. Lengo la somo hili ni kumwezesha mwalimu tarajali kuwa na uweledi na umahiri wa kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kuhesabu, kusoma, kuandika, afya na mazingira pamoja na sanaa na michezo. Somo hili linamjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo ambao utamwezesha kuwa mbunifu na mnyumbufu katika ufaraguzi wa teknolojia na vifaa vingine saidizi sahili katika ufundishaji na ujifunzaji, uchopekaji wa masuala mtambuka na matumizi ya mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ufundishaji wa Elimu ya Awali na Darasa la I – II.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mkufunzi kumwandaa mwalimu tarajali kufundisha Elimu ya Awali na Darasa la I – II Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali wa Mwaka 2023. Pia, muhtasari huu utamwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji zitakazomjengea mwalimu tarajali stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake ya ufundishaji na ujifunzaji.

2.0 Malengo Makuu ya Elimu

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based action research*).

4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwalimu tarajali ni:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia, TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom- based action research).*

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali umeainishwa katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Mwaka wa Kwanza na wa Pili*

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi
1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji katika Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Darasa la Pili	1.1 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za Kuhesabu
	1.2 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za Kusoma na Kuandika
	1.3 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali
	1.4 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira
	1.5 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za sanaa na michezo
	1.6 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali nje ya darasa

6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

6.2 Mwalimu tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri uliokusudiwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na changamoto ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutamthmini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

6.3 Mzazi

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na
(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji utaongozwa na ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu zinazomshirikisha mwalimu tarajali katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wa mwalimu tarajali. Mbinu hizo ni ujifunzaji shirikishi unaomwezesha mwalimu tarajali kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali, majadiliano katika vikundi na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni pamoja na majadiliano katika vikundi, igizo dhima, kazimradi, fikiri-andika-jozisha-shirikisha, changanya kete, utafiti, utunzi wa hadithi, uwasilishaji, masimulizi, michezo mbalimbali na mbinu zingine zinazohusiana kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na ufaraguzi wa zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mazingira halisi ya mwanafunzi.

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji, umri na uwezo wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kusikia na kushika zana. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka au kufaragua zana kwa kutumia makunzi/malighafi zinazopatikana katika mazingira yake. Baadhi ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni abakasi, dadu, sinia la namba, chati za namba na herufi, vibao fumbo, kadi za namba, herufi na picha, vihesabio, michoro ya picha mbalimbali, domino, ngoma, zeze, kengele, filimbi, kinanda, viongeza sauti, vikuza maandishi, zanamguso/mkwaruzo, kamusi ya lugha ya alama, alfabeti ya lugha za alama, mashine za breli na vifaa vya TEHAMA. Aidha, Mkufunzi anapaswa kuhakikisha kuwa mwalimu tarajali anapata nafasi ya kujifunza uandaaji na utumiaji wa zana mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji.

9.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia malengo ya elimu yaliyokusudiwa. Upimaji wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I – II utazingatia upimaji endelevu na tamati ili kutambua uwezo na mahitaji ya ujifunzaji wa mwalimu tarajali. Upimaji huu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Zana zitakazotumika katika upimaji ni zile zitakazozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha anampima mwalimu tarajali katika nyanja zote za upimaji ambazo ni maarifa, stadi na mwelekeo. Zana za upimaji kama vile; mitihani, majaribio, bungua bongo, mazoezi ya darasani, maswali ya papo kwa papo, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazimradi na nyingine kama hizo zitatutumika ili kuleta ufanisi katika upimaji endelevu wa ujifunzaji wa Mwalimu tarajali. Aidha, ni muhimu kufanya upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali ili kubaini kiwango cha ujifunzaji alichofikia katika nyanja zote. Matokeo ya upimaji yatasaidia kufanya uboreshaji ili kuhakikisha malengo ya Elimu ya Ualimu Stashahada ya Elimu ya Awali yamefikiwa ipasavyo.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Upimaji wa mwisho utachangia asilimia thelathini (30%) na upimaji endelevu utachangia asilimia sabini (70%). Kwa upande wa upimaji endelevu, alama za mtihani wa muhula wa pili mwaka wa kwanza itakuwa 10%, kazimradi ya ufaraguzi 15% na mafunzo kwa vitendo 45%. Aidha, alama za mafunzo kwa vitendo zitokane na ufundishaji igizi/kiduchu 20% na ufundishaji shule za jirani 25%. Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

Jedwali Na. 2: *Alama za Upimaji Endelevu*

Upimaji	Asilimia (%)
Mtihani wa Muhala wa Pili Mwaka wa Kwanza	10
Kazimradi ya Ufaraguzi	15
Ufundishaji Igizi/Kiduchu	20
Ufundishaji Shule Jirani	25
Jumla	**70**

10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I – II unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni saba (7) kwa wiki.

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Darasa la I – II umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni: umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana na idadi ya vipindi kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 3 na 4.

Mwaka wa Kwanza

Jedwali Na. 3: *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji katika Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Darasa la Pili	1.1 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za Kuhesabu	(a) Kufafanua maana na umuhimu wa stadi za awali za kuhesabu	Maana na umuhimu wa stadi za awali za kuhesabu zimefafanuliwa	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali na kadi za manila zenye maana na umuhimu wa stadi za awali za kuhesabu	84
		(b) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Matumizi ya sanaa na michezo yametumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kuhesabu	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, vitu halisi (vihesabio dadu, vizibo, vijiti, domino, zana mguso, ngoma, filimbi na vikuza maandishi), video na chati/kadi za namba	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(c) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Mbinu nyinginezo zimetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, video, vitu halisi vitu halisi (vihesabio dadu, vizibo, vijiti, domino, zana mguso, ngoma, filimbi na vikuza maandishi), kamusi ya lugha ya alama, alfabeti ya lugha za alama na chati/kadi za namba	
		(d) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Mbinu anuai zimetumika kukabiliana na darasa kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kuhesabu	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, vitu halisi (vihesabio, dadu, vizibo, vijiti, domino, zana mguso, ngoma, filimbi na vikuza maandishi), video na chati/kadi za namba	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(e) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka zimetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, machapisho, video za masuala mtambuka, vitu halisi (vihesabio, dadu, vizibo, vijiti, domino, zana mguso, ngoma, filimbi na vikuza maandishi), picha zinazohusiana na masuala mtambuka na chati za picha	
		(f) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kuhesabu	Mbinu za kuchopeka TEHAMA zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kuhesabu	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, vifaa halisi, video za mbinu za kuchopeka TEHAMA	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	1.2 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za Kusoma na Kuandika	(a) Kufafanua maana na umuhimu wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Maana na umuhimu wa stadi za awali za kusoma na kuandika umefafanuliwa	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, vitu halisi, video na kadi za manila zenye maana na umuhimu wa stadi za awali za kusoma na kuandika	98
		(b) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Sanaa na michezo imetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, video, vitu halisi (domino, zana mguso na vibao fumbo), picha na chati/kadi za herufi, silabi na maneno	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(c) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Mbinu nyinginezo zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Video, vitu halisi (domino, zana mguso, vibao fumbo, alfabeti ya lugha za alama na mashine za breli), kamusi ya lugha ya alama na chati/kadi za herufi, silabi na maneno	
		(d) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Vitu halisi (domino, zana mguso, picha na vibao fumbo), video na chati/kadi za herufi, silabi na maneno	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(e) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, majarida, video za masuala mtambuka na chati za picha	
		(f) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Mbinu za kuchopeka TEHAMA zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma na kuandika	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, vitu halisi, video na vifaa vya TEHAMA	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	1.3 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali	(a) Kumudu ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali	Ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali umefanyika	Miongozo na vitabu ya elimu ya awali, makunzi mbalimbali, video na vifaa vya TEHAMA	49
		(b) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali	Teknolojia na vifaa vingine saidizi vimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali	Vitu halisi, video, zana mguso na vifaa vya TEHAMA	

Mwaka wa Pili

Jedwali Na. 4: *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji katika Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Darasa la Pili	1.4 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira	(a) Kufafanua maana na umuhimu wa stadi za afya na mazingira	Maana na umuhimu wa stadi za afya na mazingira umefafanuliwa	Miongozo na vitabu ya elimu ya awali na picha zinazohusu afya na mazingira	105
		(b) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira	Sanaa na michezo imetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa afya na mazingira	Vifaa vya sanaa na michezo, miongozo na vitabu ya elimu ya awali, vitu halisi na chati/picha zinazohusu afya na mazingira	
		(c) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira	Mbinu nyinginezo zimetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa afya na mazingira	Vifaa vya afya na mazingira, miongozo na vitabu ya elimu ya awali, vitu halisi, video, kamusi ya lugha ya alama, mashine za	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
				breli, na chati/picha zinazohusu afya na mazingira	
		(d) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira	Mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa zimetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa afya na mazingira	Video za mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa, zana mguso, alfabeti ya lugha za alama na mashine za breli vitu halisi na chati/picha zinazohusu afya na mazingira	
		(e) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira	Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka zimetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa afya na mazingira	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, majarida na chati za picha	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(f) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za afya na mazingira	Mbinu za kuchopeka TEHAMA zimetumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa afya na mazingira	Vitu halisi, video, zana mguso na vifaa vya TEHAMA	
	1.5 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	(a) Kufafanua maana na umuhimu wa stadi za awali za sanaa na michezo	Maana na umuhimu wa stadi za awali za sanaa na michezo umefafanuliwa	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali na picha za sanaa na michezo	112
		(b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	Mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	Video za mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa, zana mguso, kamusi ya lugha ya alama, mashine za breli na chati/picha za sanaa na michezo	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(c) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	Mbinu nyinginezo zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	Vitabu na miongozo ya elimu ya awali, zana mguso, kamusi ya lugha ya alama, mashine za breli na chati/picha za sanaa na michezo	
		(d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za sanaa na michezo	Miongozo na vitabu vya elimu ya awali, majarida na chati za picha za sanaa na michezo	
		(e) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi	Mbinu za kuchopeka TEHAMA zimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi	Video za mbinu za kuchopeka TEHAMA, vitu halisi, vifaa vya TEHAMA na chati za picha za sanaa na michezo	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		za awali za sanaa na michezo	za awali za sanaa na michezo		
	1.6 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za awali nje ya darasa	(a) Kumudu matumizi ya mbinu za usimamizi wa shughuli za ujifunzaji wa stadi za awali nje ya darasa	Mbinu za usimamizi wa shughuli za ujifunzaji wa stadi za awali nje ya darasa zimetumika	Vifaa vya TEHAMA, vitabu, Miongozo na vitabu vya elimu ya awali, vifani na chati za picha	28

Bibliografia

Brookhart, S.M. (2008). *How to give effective feedback to your students*. ASCD publications.

Brookhart, S. M., & McMillan, J. H. (Eds). (2019). *Classroom assessment and educational measurement*. Routledge.

Harju- Luukkainen, H. (2021) *Early Childhood education in Finland – from policy to practice (Play as a source of development, learning and well-being)*. Springer.

Levin, J., & Nolan, J. F. (2000). *Principles of classroom management: A professional decision-making model*. Allyn and Bacon.

Mohan, R. (2016). *Measurement, evaluation and assessment in education*. PHI Learning Pvt. Ltd.

Orlich, D. C., Harder, R. J., Callahan, R. C., Trevisan, M. S., & Brown, A. H. (2012). *Teaching strategies: A guide to effective instruction*. Cengage Learning.

Sood, N. (2016). *Guidance counselling education*. Vikas Publishing House Pvt. Ltd.

Sundaram, G. (2007). *Principles and practice of guidance and counselling*. Aavishkar Publisher Distributors.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019): *Mwongozo wa mwalimu wa kufundishia elimu ya awali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.